TANGAZO LA SERIKALI NA. 466 la tarehe 25/7/2025

SHERIA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI,
(NA. 6 YA MWAKA 2025)

# KANUNI

## KANUNI ZA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI ZA MWAKA 2025

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Fasili.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YANAYOHUSU KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UWEKEZAJI NA KAMATI YA WATAALAMU

3. Kamati ya Wataalamu.
4. Vikao vya Kamati ya Wataalamu.
5. Majukumu ya Kamati ya Wataalamu.
6. Sekretarieti ya Kamati ya Wataalamu.
7. Maombi ya uwekezaji wa kimkakati.
8. Uwasilishaji wa masuala yanayohusiana na uwekezaji.
9. Utaratibu wa kutoa uamuzi wa maombi ya uwekezaji wa kimkakati.
10. Utaratibu wa kuongeza muda wa vivutio vya ziada.

SEHEMU YA TATU
USAJILI WA WAWEKEZAJI NA UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI

11. Maombi ya usajili wa wawekezaji.

12. Kukataliwa kwa Maombi.
13. Maombi ya cheti.
14. Masharti ya utoaji cheti au leseni.
15. Muda wa uhalali wa cheti.
16. Mabadiliko ya jina au umiliki.
17. Mabadiliko yasiyoathiri manufaa.
18. Maombi ya kuhuisha cheti.
19. Utaratibu wa kufuta cheti au leseni.
20. Madhara ya kufutwa kwa cheti au leseni.

SEHEMU YA NNE
UHAMASISHAJI, UWEZESHAJI NA URATIBU WA MASUALA YA UWEKEZAJI

21. Mpango wa kuhamasisha uwekezaji.
22. Utekelezaji wa mpango wa kuhamasisha uwekezaji.
23. Huduma kupitia maafisa waliowekwa kwenye Mamlaka.
24. Utoaji wa hati zisizo za asili kwa wawekezaji.
25. Vibali vya kazi na ukaazi.
26. Ufuatiliaji na tathmini ya miradi.
27. Taarifa ya mwaka ya mwekezaji.
28. Matumizi ya hati isiyo ya asili kama dhamana.

SEHEMU YA TANO
UWEKEZAJI KATIKA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI
*(a) Masharti yanayohusiana na utengaji na utangazaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

29. Maombi ya kutenga na kutangaza eneo maalumu la kiuchumi.
30. Utangazaji wa eneo katika Gazeti la Serikali.
31. Taarifa kwa mwombaji.
32. Udhibiti wa bidhaa na shughuli katika eneo maalumu la kiuchumi.

*(b) Masharti yanayohusiana na uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

33. Maombi ya leseni ya uendelezaji.
34. Leseni ya Uendelezaji.
35. Muda wa kuanza shughuli za uendelezaji.
36. Uwasilishaji wa taarifa.

37. Cheti cha Kukamilika Ujenzi.
38. Wajibu wa mwendelezaji.

*(c) Masharti yanayohusiana na uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

39. Maombi ya leseni ya uendeshaji.
40. Leseni ya uendeshaji.
41. Masharti ya leseni ya uendelezaji.
42. Uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi.
43. Wajibu wa mwendeshaji.
44. Ukiukaji wa masharti ya leseni ya uendeshaji.

*(d) Masharti yanayohusiana na uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje*

45. Maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje.
46. Utoaji wa leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje.
47. Uwasilishaji wa taarifa ya robo mwaka.
48. Wajibu wa kutunza na kutoa taarifa.

*(e) Masharti yanayohusiana na uzalishaji kwa ajili soko la ndani*

49. Maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
50. Ukaguzi wa eneo la uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
51. Leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
52. Haki na wajibu wa mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
53. Hatua dhidi ya ukiukwaji wa masharti ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
54. Notisi ya kutotekeleza masharti ya leseni.

*(f) Masharti yanayohusiana na watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi*

55. Maombi ya kibali cha kutoa huduma.
56. Kibali cha mtoa huduma.
57. Mtoa huduma kutostahili kupata vivutio.
58. Mamlaka ya kutoza kodi ya pango.

SEHEMU YA SITA
VIVUTIO VYA UWEKEZAJI KATIKA ENEO MAALUMU LA KIUCHUMI

59. Vivutio vya mwendelezaji.
60. Vivutio vya mwendeshaji.
61. Vivutio vya mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
62. Masharti ya utoaji vivutio kwa mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.
63. Vivutio vya mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA KUJITOA AU KUBADILISHA SHUGHULI YA UZALISHAJI KATIKA ENEO MAALUMU LA KIUCHUMI

64. Kubadilisha shughuli ya uzalishaji.
65. Haki ya Mamlaka kununua au kutonunua majengo.
66. Mamlaka kusimamia uuzaji wa majengo.
67. Uzingatiaji wa sheria katika uuzaji wa majengo

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI YA JUMLA

68. Ufutaji au usitishaji wa leseni au kibali.
69. Zuio la kuongeza msamaha wa kodi.
70. Zuio dhidi ya kufanya shughuli zisizo na leseni.
71. Mamlaka kuamua aina ya bidhaa zitakazozalishwa.
72. Zuio la kuingia au kufanya shughuli kwenye eneo maalumu la uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje.
73. Usimamizi wa mazingira .
74. Mwongozo wa Usanifu wa Ujenzi wa Miundombinu.
75. Notisi ya kurekebisha miundombinu.
76. Ada na tozo.
77. Usiri wa taarifa.
78. Rufaa.
79. Mapitio.
80. Ushughulikiaji wa malalamiko.
81. Uharibifu wa mali.
82. Kufutwa kwa Kanuni

________

MAJEDWALI

________

SHERIA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI
(NA. 6 YA 2025)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 50)*

KANUNI ZA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI ZA MWAKA 2025

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi za Mwaka 2025.

Fasili

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria;

"cheti" maana yake ni cheti cha uwekezaji kinachotolewa na Mamlaka kwa mwekezaji anayewekeza katika eneo lililo nje ya eneo maalumu la kiuchumi kwa kuzingatia masharti ya Sheria;

"eneo la forodha" maana yake ni eneo lililoteuliwa kama eneo la forodha kwa mujibu wa sheria inayosimamia masuala ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

"eneo maalumu la kiuchumi" maana yake ni eneo la ardhi lililoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha Sheria;

"eneo maalumu la uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje" maana yake ni eneo maalumu la kiuchumi lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria, ambalo liko nje ya eneo la forodha

na limebainishwa kama eneo linalodhibitiwa na mamlaka ya forodha kwa madhumuni ya kufanya shughuli za uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje ambalo linaweza kuwa eneo la kiwanda kimoja au eneo la viwanda vingi;

"Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji" maana yake ni Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria;

"Kamati ya Wataalamu" maana yake ni Kamati ya Wataalamu iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria;

"leseni" maana yake ni idhini iliyotolewa na Mamlaka kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu, uendeshaji au uzalishaji katika eneo maalumu la uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya soko la ndani au la nje;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"mtoa huduma" maana yake ni mmiliki wa kibali cha utoaji huduma katika eneo maalumu la kiuchumi;

"mwendelezaji" maana yake ni mmiliki wa leseni ya uendelezaji wa miundombinu ya eneo maalumu la kiuchumi;

"mwendeshaji" maana yake ni mmiliki wa leseni ya uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi;

"mzalishaji" maana yake ni mmiliki wa leseni ya uzalishaji wa bidhaa katika eneo maalumu la kiuchumi kwa ajili ya mauzo ya soko la ndani au la nje;

"Sekretarieti" maana yake ni Sekretarieti ya Kamati ya Wataalamu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji;

Sheria Na. 6 ya 2025

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi;

"soko la ndani" maana yake ni soko ambalo lipo au linapatikana katika katika eneo la forodha;

"soko la nje" maana yake ni soko lingine lolote ambalo halipo katika eneo la forodha; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya uwekezaji.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YANAYOHUSU KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UWEKEZAJI NA KAMATI YA WATAALAMU

Kamati ya Wataalamu

3.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 7 cha Sheria, Kamati ya Wataalamu itakuwa na wajumbe kumi wafuatao:

(a) Naibu Katibu Mkuu anayehusika na usimamizi wa sera kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha, atakayekuwa Mwenyekiti;

(b) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, ambaye atakuwa Katibu;

(c) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya uwezeshaji wa uwekezaji kutoka Mamlaka;

(d) Kamishna anayehusika na masuala ya Sera kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha;

(e) Kamishna wa Ardhi;

(f) Mkurugenzi wa Divisheni ya Mikataba kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(g) Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(h) Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(i) Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uwekezaji kutoka Wizara yenye dhamana na uwekezaji;

(j) Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara yenye dhamana ya uwekezaji; na

(k) Mkurugenzi wa Idara ya inayohusika na Mtangamano wa Biashara kutoka Wizara yenye dhamana na viwanda.

(2) Kamati ya Wataalamu inaweza kualika mtu mwenye ujuzi kutoka sekta inayohusiana na suala linalojadiliwa kwa ajili ya ushauri wa kitaalamu.

Vikao vya Kamati ya Wataalamu

4.-(1) Kamati ya Wataalamu itakutana angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(2) Kamati ya Wataalamu itaweka utaratibu wa kuendesha shughuli zake.

(3) Akidi katika kikao cha Kamati ya Wataalamu itakuwa zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wa Kamati ya Wataalamu.

Majukumu ya Kamati ya Wataalamu

5.-(1) Kamati ya Wataalamu itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupokea na kuchakata maombi ya vivutio vya ziada vya kikodi na visivyo vya kikodi na kuishauri Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji;

(b) kupokea na kuchakata masuala mbalimbali yanayolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuishauri Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji; na

(c) kutekeleza jukumu lingine lolote kadri ambavyo Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji itakavyoelekeza.

(2) Kamati ya Wataalamu inaweza kualika mwombaji wa vivutio na kusikiliza maombi yake na Kamati itazingatia Kanuni hizi wakati wa utoaji mapendekezo.

Sekretarieti ya Kamati ya Wataalamu

6.-(1) Sekretarieti ya Kamati ya Wataalamu itakuwa na wajumbe kumi na mbili kama ifuatavyo:

(a) wajumbe wawili kutoka Wizara yenye dhamana ya uwekezaji, ambapo mmoja wao atakuwa mwenyekiti;
(b) wajumbe wawili kutoka Mamlaka ambapo mmoja wao atakuwa katibu;
(c) mjumbe kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Uratibu;
(d) mjumbe kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya Fedha, Idara ya Sera;
(e) mjumbe kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya Viwanda, Idara ya Mtangamano wa Biashara;
(f) mjumbe kutoka Wizara yenye dhamana na masuala ya ardhi, Ofisi ya Kamishna wa Ardhi; na
(g) wajumbe wanne kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania ambao watatoka katika Idara ya Walipa kodi wakubwa, Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa, Idara ya Kodi za ndani na Idara ya Sheria.

(2) Sekretarieti ina wajibu wa kuiwezesha Kamati ya Wataalamu kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika kanuni ya 5.

Maombi ya uwekezaji wa kimkakati

7.-(1) Mtu anayekusudia kuwa mwekezaji wa kimkakati atafanya maombi ya hadhi ya uwekezaji wa kimkakati kwa Katibu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji kwa kutumia Fomu Na.1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza pamoja na malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi chini ya kanuni hii yataambatishwa na nyaraka zifuatazo:

(a) nakala ya cheti cha uwekezaji au leseni;

(b) upembuzi wa mradi ukionesha gharama, faida kwa taifa na kwa mwekezaji, vivutio vya ziada anavyoomba katika Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ili kumwezesha kutekeleza mradi kikamilifu;

(c) maelezo mafupi yanayoonesha masuala ya msingi yaliyoainishwa ndani ya maombi ya mwekezaji kama yalivyotajwa katika aya (b); na

(d) uthibitisho wa malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 21 cha Sheria, maombi chini ya kanuni hii yatakubaliwa ikiwa eneo ambalo mwekezaji anawekeza linashabihiana na kuchagiza vipaumbele vya kitaifa vya maendeleo ya kiuchumi, hususani vigezo vifuatavyo vitazingatiwa:

(a) uwezo wa kuzalisha ajira kwa wingi na kuchagiza uzalishaji wa ajira zaidi katika sekta nyingine ambazo zinategemeana;

(b) uwezo wa kuongeza mauzo ya nje kwa bidhaa na huduma zinazohitajika katika masoko ya nje, na zenye uwezo wa kuunganisha soko la ndani na la nje;

(c) uwezo wa kuchochea ukuaji wa sekta nyingine, ambazo uzalishaji wake ni chachu ya uzalishaji katika sekta nyingine;

(d) uwezo wa kuongeza thamani ya malighafi za ndani na bidhaa kuongezwa thamani kabla ya kumfikia mtumiaji;

(e) uwezo wa kukuza mapato kwa kuwekeza katika sekta ambazo zina uwezo wa kuzalisha na kukuza vyanzo vya mapato kwa wingi na endelevu;

(f) uwezo wa kuchochea uzalishaji kwa kuanzisha kongani za kiuchumi kwenye maeneo ya kipaumbele, kijiografia na katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi;
(g) uwezo wa kuongeza ujuzi au utaalamu kwa kuhawilisha teknolojia kwa watanzania; au
(h) uwezo wa kuzalisha bidhaa au kutoa huduma muhimu kwa maendeleo katika sekta za kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia vipaumbele kwa wakati huo.

(5) Pamoja na vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria, miradi ya kipaumbele kwa ajili ya hadhi ya uwekezaji wa kimkakati ni pamoja na-
(a) viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya chakula au biashara, mifugo, uvuvi na bidhaa za misitu;
(b) kilimo cha kuzalisha mazao ya chakula au biashara, ufugaji, uvuvi, misitu kwa kushirikiana na wakulima wadogo;
(c) miradi ya ujenzi wa viwanda, viwanda vinavyotumia nishati kubwa na uzalishaji wa kemikali zisizo hatarishi;
(d) ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya mawasiliano, nishati , gesi asilia, huduma za afya, elimu, utalii, michezo na usafirishaji;
(e) viwanda vya kuunganisha na kuzalisha bidhaa za magari, boti, mitambo, vipuri vya mitambo na magari, madawa ya binadamu au mifugo na pembejeo za kilimo; au
(f) sekta nyingine mpya za kimkakati zitakazojitokeza.

Uwasilishaji wa masuala yanayohusiana na uwekezaji

8. Mwekezaji anaweza kuwasilisha masuala yanayohusiana na uwekezaji isipokuwa migogoro kwa Katibu wa Kamati ya Taifa ya

Maendeleo ya Uwekezaji kupitia Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza pamoja na uthibitisho wa malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Utaratibu wa kutoa uamuzi wa maombi ya uwekezaji wa kimkakati

9.-(1) Katibu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji atawasilisha maombi ya uwekezaji wa kimkakati na masuala mengine kwa Kamati ya Wataalamu kwa ajili ya kuchakatwa.

(2) Kamati ya Wataalamu itawasilisha mapendekezo kwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji katika kipindi cha siku kumi na nne baada ya kukamilika kwa uchakataji wa maombi na masula mengine yaliyowasilishwa.

(3) Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji itafanya uamuzi kuhusiana na mapendekezo yaliyowasilishwa, na Katibu atatoa taarifa ya uamuzi huo kwa mwombaji au mwasilishaji wa suala husika.

Utaratibu wa kuongeza muda wa vivutio vya ziada

10.-(1) Mwekezaji wa kimkamkati aliyepewa vivutio vya ziada anaweza kuomba kuongezewa muda wa kutumia vivutio hivyo kwa kuwasilisha barua kwa Katibu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji akiainisha sababu za msingi za maombi hayo katika kipindi kisichopungua miezi mitatu (3) kabla ya kuisha kwa muda wa awali.

(2) Katibu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji atawasilisha maombi yaliyoletwa chini ya kanuni hii kwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji kwa ajili ya uamuzi.

(3) Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji katika ufanyaji uamuzi, pamoja na masuala mengine, itazingatia iwapo kulikuwa na ucheleweshaji katika upatikanaji wa ardhi ya mradi, mtaji, vibali pamoja na leseni mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji.

SEHEMU YA TATU

## USAJILI WA WAWEKEZAJI NA UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI

Maombi ya usajili wa wawekezaji

11.-(1) Mtu anayekusudia kufanya uwekezaji atafanya maombi ya usajili kwa Mamlaka kwa kutumia Fomu Na. 3 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza pamoja na kufanya malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi ya usajili wa mwekezaji yatajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) jina na anwani ya mwombaji;
(b) aina ya shughuli ya uwekezaji inayopendekezwa na eneo linalopendekezwa ambapo shughuli hiyo itafanyika;
(c) mchanganuo wa mtaji unaopendekezwa au kiasi cha uwekezaji;
(d) idadi ya ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zitakazozalishwa na uwekezaji; na
(e) uthibitisho wa malipo ya ada za usajili.

(3) Mamlaka itafanyia kazi maombi yaliyowasilishwa na inaweza kutoa cheti cha usajili kwa mwombaji aliyekidhi vigezo na masharti ndani ya siku kumi na nne za kazi.

Kukataliwa kwa Maombi

12. Endapo Mamlaka itakataa maombi chini ya Kanuni hizi, itamtaarifu mwombaji na kumpa sababu za maombi yake kukataliwa ndani ya siku saba.

Maombi ya cheti

13.-(1) Maombi ya cheti yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa kutumia Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la kwanza pamoja na malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi ya cheti yatajumuisha taarifa zifuatazo-

(a) jina na anwani ya taasisi ya kibiashara inayopendekezwa, hadhi yake kisheria, taarifa za benki, majina na anwani za

kila mkurugenzi au mbia na jina, anwani, utaifa na umiliki wa hisa kwa kila mwanahisa;

(b) sifa, uzoefu na maelezo mengine muhimu ya wasimamizi wa mradi;

(c) aina ya shughuli ya kibiashara inayopendekezwa na eneo linalopendekezwa ambapo shughuli hiyo itafanyika;

(d) mchanganuo wa mtaji unaopendekezwa au kiasi cha uwekezaji na makadirio ya ukuaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo;

(e) taarifa ya namna uwekezaji utakavyofadhiliwa; na

(f) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi.

(3) Endapo maombi ni kwa ajili ya kukarabati au kupanua biashara iliyopo au vyote kwa pamoja, yataambatishwa na-

(a) jina la biashara iliyopo na Katiba yake;

(b) sifa za wasimamizi wa mradi;

(c) taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa miaka mitatu iliyopita au kipindi kingine chochote kitakachoainishwa kwa biashara ambayo haijatimiza miaka mitatu tangu kuanzishwa;

(d) aina ya ukarabati au upanuzi;

(e) mchanganuo wa mtaji na makadirio ya ukuaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo;

(f) ufadhili wa mradi wa ukarabati au upanuzi, pamoja na uthibitisho wa upatikanaji wa fedha; na

(g) tamko kwamba upanuzi au ukarabati utatekelezwa kama ilivyooneshwa kwenye makadirio.

(4) Mamlaka itachakata maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni hii na inaweza-

(a) kukubali ombi na kuthibitisha taasisi ya kibiashara; au
(b) kukataa ombi hilo.

(5) Endapo Mamlaka imekubali ombi na kuithibitisha taasisi ya kibiashara chini ya kanuni ndogo ya (4)(a), itatoa cheti cha uwekezaji kwa taasisi iliyothibitishwa.

(6) Endapo Mamlaka itakataa ombi chini ya kanuni hii itamtaarifu mwombaji na kutoa sababu za kukataa.

Masharti ya utoaji cheti au leseni

14.-Mamlaka inaweza kutoa cheti au leseni kwa mwombaji iwapo biashara-
(a) inamilikiwa na mwekezaji wa kigeni au ikiwa ni ubia, ina kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji usiopungua shilingi za Tanzania bilioni moja na milioni mia tano (1,500,000,000/=); au
(b) inamilikiwa na Mtanzania, ina kima cha chini cha mtaji wa uwekezaji usiopungua shilingi za Tanzania milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=).

Muda wa uhalali cheti

15.-(1) Cheti kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano.

(2) Cheti kitakuwa ni uthibitisho kwamba masharti ya Sheria na Kanuni hizi yamezingatiwa.

Mabadiliko ya jina au umiliki
Sura za 212 na 213

16. Mamlaka inaweza kutoa cheti baada ya kupokea uthibitisho wa mabadiliko yaliyofanyika na mwekezaji kuhusiana na jina la biashara au umiliki wa mtaji kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, au sheria nyingine yoyote.

Mabadiliko yasiyoathiri manufaa

17. Kwa kuzingatia sharti linalohusu kiwango cha chini cha mtaji katika Sheria, mabadiliko yoyote yaliyorejewa katika kanuni ya 17 hayataathiri haki yoyote au wajibu wa biashara.

Maombi ya kuhuisha cheti

18.-(1) Mwekezaji mwenye cheti anaweza kufanya maombi ya kuhuisha cheti kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza angalau miezi mitatu kabla ya cheti cha awali kuisha muda.

(2) Cheti kinaweza kuhuishwa kwa kipindi kimoja tu.

(3) Mamlaka itachakata maombi ya kuhuisha cheti ndani ya siku saba za kazi tangu tarehe ya kupokea maombi husika na kumjulisha mwombaji kwa maandishi kuhusu uamuzi huo.

Utaratibu wa kufuta cheti au leseni

19.-(1). Mamlaka inaweza kufuta cheti au leseni baada ya kujiridhisha kwamba mwekezaji amekiuka masharti ya kifungu cha 17 (2) cha Sheria.

(2) Mamlaka, baada ya kubaini uwepo wa sababu za kufuta cheti au leseni, kabla ya kufuta cheti hicho, itampa mmiliki wa cheti notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta cheti au leseni.

(3) Endapo mmiliki wa cheti au leseni hajawasilisha utetezi kuhusiana na kusudio la kufuta cheti au leseni ndani ya muda ulioanishwa, Mamlaka itafuta cheti au leseni na kumtaarifu mmiliki wa cheti au leseni kuhusu uamuzi huo.

Madhara ya kufutwa kwa cheti au leseni

20. Mamlaka ikifuta cheti au leseni, mwekezaji hatoendelea kupata vivutio vilivyotolewa kwake kutokana na yeye kuwa mmiliki wa cheti au leseni.

## SEHEMU YA NNE
## UHAMASISHAJI, UWEZESHAJI NA URATIBU WA MASUALA YA UWEKEZAJI

Mpango wa kuhamasisha uwekezaji

21.-(1) Mamlaka itaandaa mpango wa kuhamasisha uwekezaji kila mwaka wa fedha na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya idhini.

(2) Bodi itawasilisha Mpango huo kwa Waziri kwa ajili ya kupata idhini na kwa kuzingatia maelekezo ya Waziri, Bodi itachukua

hatua zote zinazohitajika ili kuhakikisha kuwa mpango wa kuhamasisha uwekezaji unatekelezwa.

Utekelezaji wa mpango wa kuhamasisha uwekezaji

22.-(1) Kwa madhumuni ya kutekeleza mpango wa kuhamasisha uwekezaji, Mamlaka-

(a) itatangaza nchi kama kivutio cha uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa kusambaza taarifa, kuandaa shughuli zinazojumuisha umma na kutangaza fursa za uwekezaji ili kujenga na kuboresha taswira ya Tanzania kama nchi nzuri ya uwekezaji;

(b) itaweka katika mapitio hatua iliyofikiwa katika malengo na madhumuni ya Sheria na kuchapisha ripoti na kutoa taarifa kwa madhumuni ya kuongeza uelewa kwa mwekezaji na umma kuhusu maendeleo hayo na changamoto na masuluhisho yaliyopo kuhusiana na mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania; na

(c) kuendeleza maarifa ya kitaaluma, ujuzi na uwezo mwingine wa kitaalamu wa kuishauri Serikali kuhusu uhamasishaji wa masuala ya uwekezaji na masuala mengine yanayohusiana na uwekezaji.

Huduma kupitia maafisa waliowekwa kwenye Mamlaka

23. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 12(2) cha Sheria, maafisa wa idara mbalimbali za Serikali wanaotoa huduma katika Kituo cha Huduma Mahala Pamoja wataratibu na kusaidia uchakataji wa vibali na leseni na kutoa vibali na leseni ndani ya siku saba za kazi baada ya kupokea maombi hayo.

Utoaji wa hati zisizo za asili kwa wawekezaji

24.-(1) Mamlaka itapokea na kushughulikia maombi ya hati zisizo za asili kwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji.

(2) Mamlaka itashughulikia maombi hayo na inaweza kutoa kwa mwekezaji hati isiyo asili ya ardhi iliyoidhinishwa.

Vibali vya kazi na ukaazi

25. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 12 (1) cha Sheria, Mamlaka kupitia Kituo cha Huduma Mahala Pamoja itasaidia wawekezaji kupata vibali vya makazi, vyeti vya usajili wa biashara na leseni pamoja na vibali vingine baada ya kupokea maombi hayo.

Ufuatiliaji na tathmini ya miradi

26.-(1) Mamlaka itafanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria.

(2) Mamlaka itaandaa mpangokazi wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Bodi kila robo mwaka.

(3) Bodi itawasilisha kwa Waziri taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa mpangokazi ndani ya miezi miwili baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha.

(4) Mamlaka itatoa taarifa kwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa miradi.

Taarifa ya mwaka ya mwekezaji

27.-(1) Mwekezaji mwenye cheti atawasilisha taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi kila mwaka kwa Mamlaka.

(2) Taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi itawasilishwa kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 5 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza pamoja na malipo ya ada yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Matumizi ya hati isiyo ya asili kama dhamana
Sura ya 113

28.-(1) Kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi, mwekezaji anaweza kutumia hati isiyo asili kama dhamana ya mkopo kutoka katika benki za ndani kwa kutumia Fomu Na. 6 iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza baada ya kufanya malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Maombi ya kutumia hati isiyo asili kama dhamana ya mkopo yataambatanishwa na-

(a) uthibitisho wa maendeleo ya mradi ambao si chini ya asilimia 60 ya mradi;
(b) taarifa ya maendeleo ya mradi ambao mkopo unatumika;
(c) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi; na
(d) hati nyingine yoyote au mahitaji kama Mamlaka itakavyoamua ;

(3) Mamlaka inaweza, baada ya kufanya tathmini na uhakiki wa mradi, kutoa ridhaa kwa mwombaji kwa kuzingatia kanuni na masharti ya hati isiyo ya asili husika.

## SEHEMU YA TANO
## UWEKEZAJI KATIKA MAENEO MAALUMU YA KIUCHUMI

### *(a) Masharti yanayohusiana na utengaji na utangazaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

Maombi ya kutenga na kutangaza eneo maalumu la kiuchumi

29.-(1) Mtu anayekusudia eneo lake litengwe na kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi atafanya maombi kwa Mamlaka kwa kujaza Fomu Na. 7 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi chini ya kanuni hii yataambatishwa na-

(a) nakala ya hati miliki ya eneo husika, uthibitisho wa umiliki au mkataba wa upangishaji usiopungua miaka mitano kwa eneo la kiwanda kimoja na miaka 10 kwa eneo la viwanda vingi;
(b) nakala ya namba ya mlipa kodi na namba ya usajili ya kodi ya ongezeko la thamani;
(c) andiko dhana linaloainisha upembuzi yakinifu, mpango mkakati, mpango wa kifedha unaobainisha gharama za usanifu, ujenzi, uendelezaji,

matengenezo na uhamasishaji au utangazaji wa eneo husika;
(d) kiapo kinachothibitisha kwamba eneo hilo halina zuio au mgogoro wowote;
(e) ramani inayoonesha njia zote za kufika na kutoka katika eneo;
(f) maelezo yenye ufafanuzi wa aina ya eneo maalumu la uwekezaji linalotarajiwa kuanzishwa, yakikujumuisha aina za shughuli zitakazofanyika;
(g) barua ya utambulisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri; na
(h) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili.

(3) Mamlaka itajiridhisha na masuala yafuatayo kabla ya kupendekeza eneo kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi:
(a) kuwa eneo linalopendekezwa, halina vikwazo ama mgogoro wowote;
(b) eneo linalopendekezwa linaendana na mpango wa matumizi ya ardhi kwa eneo hilo na linafaa kwa uanzishwaji wa maeneo ya maalumu ya kiuchumi na shughuli za viwanda;
(c) aina ya uwekezaji unaopendekezwa unawiana na vipaumbele vya kitaifa vya maendeleo ya kiuchumi;
(d) mpango wa biashara uliowasilishwa kwa ajili ya maombi ya utengaji na utangazaji wa eneo unazingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi na kuonesha uwezekano wa mafanikio ya kibiashara katika eneo ikiwa ni pamoja na kubainisha kama eneo

litakuwa la kiwanda kimoja au viwanda vingi;
(e) uthibitisho wa uwezo wa kuendeleza eneo ukijumuisha uwezo wa kifedha; na
(f) iwapo mwombaji siyo mmiliki wa ardhi inayopendekezwa kutengwa na kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi awasilishe mkataba wa pango uliyosajiliwa usiopungua muda wa miaka mitatu ambao unaweza kuhuishwa.

(4) Mamlaka, baada ya kupokea maombi itayachakata na iwapo yana dosari yoyote, itamjulisha mwombaji ndani ya siku kumi na nne za kazi tangu siku ya kupokea maombi.

(5) Mamlaka inaweza kumuelekeza mwombaji kurekebisha maombi na kutoa taarifa za ziada kadri itakavyoona inafaa.

Utangazaji wa eneo katika Gazeti la Serikali

30.-(1) Mamlaka baada ya kujiridhisha kwamba maombi yamezingatia masharti ya Kanuni hizi itawasilisha maombi hayo kwa Bodi kwa ajili ya idhini.

(2) Bodi itapitia maombi na inaweza kuidhinisha au kukataa maombi hayo.

(3) Mamlaka itawasilisha kwa Waziri maombi ya utengaji wa eneo yaliyoidhinishwa na Bodi kwa ajili ya idhini na utangazaji wa notisi katika Gazeti la Serikali itakayoainisha taarifa zifuatazo-

(a) jina la eneo maalumu la kiuchumi na mipaka yake;
(b) aina ya eneo maalumu la kiuchumi linaloanzishwa;
(c) aina ya shughuli zinazotarajiwa kufanyika katika eneo maalumu la kiuchumi; na
(d) taarifa yoyote kadri itakavyohitajika na Mamlaka.

Taarifa kwa mwombaji

31.-(1) Mamlaka itamtaarifu mwombaji kwa barua siku saba baada ya eneo lake kutangazwa kuwa eneo maalumu la kiuchumi.

(2) Mamlaka itamjulisha mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa ndani ya siku 7 baada ya uamuzi huo kufanyika.

Udhibiti wa bidhaa na shughuli katika eneo maalumu la kiuchumi

32. (1) Mamlaka itasimamia na kudhibiti maeneo maalumu ya kiuchumi yanayomilikiwa na mtu binafsi au yanayomilikiwa na Mamlaka.

(2) Mamlaka inaweza kutoa notisi ya -

(a) kuzuia au kudhibiti uingizaji wa bidhaa au aina za bidhaa, huduma au malighafi kwenye eneo maalumu la kiuchumi; au

(b) kumtaka mwendelezaji, mwendeshaji, mzalishaji, mtoa huduma au mtu yeyote katika eneo hilo, kuondoa kitu chochote, bidhaa au kusimamisha shughuli zozote katika eneo maalumu la kiuchumi ndani ya muda ulioainishwa katika notisi.

(3) Mtu ambaye amepewa notisi, anaweza kuwasilisha maelezo ya utetezi kwa Mamlaka kuhusu notisi aliyopewa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokea notisi hiyo.

(4) Endapo Mamlaka itapokea wasilisho la maandishi na kuthibitisha uamuzi wake wa awali, Mamlaka itatoa taarifa ya uamuzi huo na mtu ambaye uamuzi huo umetolewa dhidi yake atatakiwa kutekeleza uamuzi huo ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea notisi hiyo.

(5) Mtu ambaye hatotekeleza uamuzi wa Mamlaka, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika-

(a) ikiwa ni mtu binafsi, atatozwa faini isiyopungua milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka minne au vyote; au

(b) ikiwa ni kampuni, itatozwa faini isiyopungua milioni kumi na tano na isiyozidi milioni hamsini.

*(b) Masharti yanayohusiana na uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

Maombi ya leseni ya uendelezaji

33.-(1) Mtu anayekusudia kufanya uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kufanya maombi ya leseni ya uendelezaji kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 8 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya leseni ya uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi yataambatishwa na-

(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni;
(b) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;
(c) uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutoka benki ya mwombaji;
(d) jina la mkandarasi na mshauri elekezi pamoja na nakala ya mikataba yao;
(e) mchoro wa eneo litakaloendelezwa ukijumuisha majengo yanayopendekezwa kuendelezwa pamoja na orodha na gharama ya vifaa vya ujenzi;
(f) mpango kazi unaopendekezwa ukijumuisha muda wa usanifu, ujenzi na kuanza kwa uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi;
(g) mpango kabambe wa eneo maalumu la kiuchumi na upembuzi yakinifu ukijumuisha taarifa zifuatazo:
    (i) uchambuzi wa kiwango cha urejesho wa kiuchumi na kifedha, ikiwa ni pamoja na gharama na manufaa ya umma,

pamoja na kiwango cha urejesho wa ndani wa eneo maalumu la kiuchumi linalopendekezwa;

(ii) taarifa kuhusu matokeo ya biashara ya kimataifa ikijumuisha thamani ya uuzaji wa bidhaa nje ya nchi na mnyororo wa thamani wa eneo maalumu la kiuchumi;

(iii) taarifa za miundombinu inayotakiwa kujengwa ndani au karibu na eneo maalumu la kiuchumi ikijumuisha miundombinu katika eneo maalumu la kiuchumi au nje ya eneo hilo la kiuchumi;

(iv) ramani au mpango wa usanifu wa jengo unaoonesha umbali wa mita tano kati ya eneo maalumu la kiuchumi na eneo la forodha;

(v) uthibitisho wa uwezo wa kifedha kuendesha mradi; na

(vi) uwezo wa kitaalamu na uzoefu katika uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi; na

(h) taarifa nyingine kadri Mamlaka itakavyoona inafaa.

Leseni ya Uendelezaji

34.-(1) Mamlaka, baada ya kujiridhisha kwamba mwombaji ametimiza masharti ya kanuni hizi, itatoa leseni ya uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi kupitia Fomu Na. 9 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Leseni ya uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi itakuwa halali kwa kipindi cha miaka miwili iwapo eneo ni la uendelezaji wa kiwanda kimoja na miaka mitano iwapo eneo ni la uendelezaji wa viwanda vingi.

(3) Maombi ya uhuishaji wa leseni ya uendelezaji yatawasilishwa kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 10 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Muda wa kuanza kwa shughuli za uendelezaji

35.-(1) Mwendelezaji ataanza ujenzi wa miundombinu katika eneo maalumu la kiuchumi ndani ya miezi sita kuanzia tarehe aliyopewa leseni ya uendelezaji.

(2) Mwendelezaji anapaswa kuwa na kibali cha ujenzi kinachotolewa na Mamlaka pamoja na cheti cha tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kabla ya kuanza ujenzi.

(3) Mamlaka itasimamia utekelezaji na uendelezaji wa miundombinu ya eneo maalumu la kiuchumi kulingana na mipango na michoro iliyoidhinishwa.

Uwasilishaji wa taarifa

36.-(1) Mwendelezaji atawasilisha kwa Mamlaka taarifa za maendeleo ya ujenzi kwa kila robo mwaka.

(2) Mwendelezaji atawasilisha taarifa inayoainisha kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu katika eneo la maalumu la kiuchumi kwa Mamlaka baada ya kukamilika kwa ujenzi.

Cheti cha Kukamilika Ujenzi

37.-(1) Mamlaka baada ya kujiridhisha na ukamilifu wa ujenzi itatoa kwa mwendelezaji Cheti cha Kukamilika kwa Ujenzi kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 11 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, na iwapo kuna kasoro katika ujenzi, Mamlaka itamtaka mwendelezaji kurekebisha kasoro hizo ndani ya muda itakaoainisha kabla ya kutoa Cheti hicho.

(2) Mwendelezaji aliyepewa Cheti cha Kukamilika kwa Ujenzi anapaswa kupata idhini ya maandishi ya Mamlaka kwa lengo la kuendeleza, kufanya mabadiliko au marekebisho ya miundombinu katika eneo maalumu la kiuchumi.

(3) Mamlaka kwa kushirikiana na mamlaka husika zitajadili mpango wa ujenzi wa miundombinu uliowasilishwa kupata namna bora ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu husika.

(4) Mamlaka au mwendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi ataingia mkataba na watoa huduma za umeme, maji, teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ajili ya utoaji wa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi.

(5) Mkataba na watoa huduma ulioainishwa katika kanuni ndogo ya 4 utajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) aina ya huduma itakayotolewa katika eneo maalumu la kiuchumi;
(b) haki na wajibu wa kila pande ya mkataba; na
(c) muda ambao huduma zitatolewa katika eneo maalumu la kiuchumi.

Wajibu wa mwendelezaji

38.-(1) Mwendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi ana haki na wajibu kama ifuatavyo:

(a) haki ya kutumia au kumiliki ardhi na mali zinazohamishika katika miundombinu ya eneo maalumu la kiuchumi;
(b) kuhamisha haki za matumizi ya ardhi au mali zinazohamishika zilizopo

katika eneo maalumu la kichumi kwenda kwa mwekezaji mwingine baada ya kupata kibali kutoka kwa Mamlaka;

(c) kuendeleza na kuongeza miundombinu katika eneo maalumu la kiuchumi;

(d) kupata vivutio vya uendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi kwa mujibu wa sheria; na

(e) kwa ridhaa ya Mamlaka, anaweza kuingia katika mkataba kwa ajili ya kufanya usanifu, uwezeshaji wa kifedha na uendendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi.

*(c) Masharti yanayohusiana na uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi*

Maombi ya Leseni ya Uendeshaji

39.-(1) Mtu anayekusudia kufanya uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kufanya maombi ya Leseni ya Uendeshaji kwa kujaza Fomu Na. 8 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya leseni ya uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi yataambatishwa na-

(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni;

(b) mpango wa uendeshaji na usimamizi wa eneo maalumu la kiuchumi;

(c) iwapo mwombaji siyo mmiliki, mkataba kati ya mwombaji na mmiliki;

(d) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;

(e) makisio ya mapato ya kikodi na yasiyo ya kikodi yanayotokana na uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi;

(f) majukumu yatakayotekelezwa na mwendeshaji katika eneo maalumu la kichumi;

(g) uthibitisho wa uzoefu wa uendeshaji na usimamizi wa eneo maalumu la kiuchumi au uzoefu unaofanana na huo;
(h) barua ya utambulisho au akaunti ya benki ya kampuni;
(i) uthibitisho wa usajili wa kodi ya ongezeko la thamani;
(j) mpango wa usimamizi wa eneo maalumu la kiuchumi unaopendekezwa ikijumuisha tozo zitakazotozwa kwa ajili ya huduma, miundombinu au huduma zitakazotolewa moja kwa moja au vinginevyo; na
(k) taarifa nyingine zozote kadri Mamlaka itakavyoona inafaa.

Leseni ya uendeshaji

40.-(1) Mamlaka, ndani ya siku 30 baada ya kupokea maombi na kujiridhisha kwamba mwombaji amekidhi vigezo, itatoa leseni ya uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi kwa mwombaji kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 12 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza .

(2) Leseni ya uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi itakuwa halali kwa kipindi cha miaka miwili.

(3) Mwendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kufanya maombi ya uhuishaji wa leseni yake na Mamlaka inaweza kuhuisha leseni hiyo kwa kipindi kingine cha miaka miwili.

(4) Maombi ya uhuishaji wa leseni yatafanyika kwa kutumia Fomu Na. 10 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, na yatafanyika angalau ndani ya miezi mitatu kabla ya leseni kuisha muda wake.

Masharti ya leseni ya uendeshaji

41.-(1) Mmiliki wa leseni ya uendeshaji atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) ataanza uendeshaji ndani ya muda ulioainishwa katika Leseni ya endeshaji;
(b) kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji, umeme, mawasiliano na huduma nyingine muhimu katika eneo maalumu la kiuchumi;
(c) kubainisha mipaka kati ya eneo maalumu la kiuchumi na eneo la forodha;
(d) kusimamia uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi;
(e) kutenga eneo litakalotumiwa na Mamlaka na mamlaka ya forodha kama ofisi kwa ajili ya uendeshaji wa kituo cha huduma mahala pamoja;
(f) kuwezesha upatikanaji wa mizani ya kupimia uzito katika malango ya kuingia eneo maalumu la kiuchumi;
(g) kuhakikisha bidhaa zinazoingia na kutoka katika eneo maalumu la kiuchumi zimekaguliwa na kuruhusiwa na mamlaka ya forodha;
(h) kutoa huduma sawa kwa wawekezaji waliopo katika eneo maalumu la kiuchumi;
(i) kuzingatia miongozo ya kiforodha inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania;
(j) kushirikiana na Mamlaka kuhamasisha uwekezaji katika eneo maalumu la kiuchumi;
(k) kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kila robo mwaka kwa Mamlaka, inayoainisha masuala yafuatayo:
    (i) idadi ya viwanja vilivyopangishwa na ambavyo havijapangishwa

katika eneo maalumu la kiuchumi ;

(ii) kiwango cha huduma muhimu zinazopatikana katika eneo maalumu la kiuchumi;

(iii) gharama za ukodishaji katika eneo maalumu la kiuchumi; na

(iv) taarifa nyingine yoyote itakayoombwa na mamlaka;

(l) kulipa ada, tozo au kodi zozote zinazotakiwa kulipwa kwa Mamlaka au mamlaka nyingine;

(m) kuhakikisha ulinzi na usalama katika eneo maalumu la kiuchumi;

(n) kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kijamii katika eneo maalumu la kiuchumi ambazo zinajumuisha huduma za afya, migahawa, chakula na huduma nyingine;

(o) kuhakikisha kuwa mpangishaji katika eneo maalumu la kiuchumi anafanya shughuli kwa kuzingatia leseni iliyotolewa na Mamlaka;

(p) kupata kibali cha ujenzi kutoka kwa Mamlaka; na

(q) kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya mwaka.

Uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi

42.-(1) Mamlaka itasimamia na kuendesha eneo maalumu la kiuchumi inalolimiliki.

(2) Mamlaka inaweza kuweka kandarasi ya usimamizi wa eneo maalumu la kiuchumi.

(3) Mmiliki wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kuweka kandarasi ya uendeshaji na

usimamizi wa eneo hilo baada ya kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mamlaka.

Wajibu wa mwendeshaji

43.-(1) Mwendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia na kuendesha eneo maalumu la kiuchumi;
(b) kukodisha viwanja katika eneo maalumu la kiuchumi kwa mtu mwenye leseni iliyotolewa na Mamlaka;
(c) kuwezesha utengenezaji au usindikaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya mauzi ya nje au soko la ndani;
(d) kuhakikisha hatua za udhibiti wa forodha zinafanyika ndani ya eneo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania;
(e) kuhakikisha kwamba miundombinu ya eneo ipo katika hali nzuri muda wote;
(f) kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msingi ikiwemo maji, umeme, gesi na miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano zinapatikana kwa urahisi katika eneo maalumu la kiuchumi;
(g) kulipa kwa Mamlaka gharama zinazohusiana na udhibiti na huduma zinazotumiwa katika eneo;
(h) kutoza kodi au ada kwa huduma zingine zinazoweza kutolewa;
(i) kutenga eneo linalotenganisha eneo maalumu la kiuchumi na eneo la forodha kwa ajili kulinda mapato pamoja na kuweka masharti nafuu ya kuwezesha usafiri wa watu, usafirishaji, vyombo vya usafiri na bidhaa zinazoingia au kutoka katika eneo hilo;

(j) kuhakikisha kuna ulinzi wa kutosha katika eneo maalumu; na
(k) kutenga ofisi kwa ajili ya kituo cha huduma mahala pamoja kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka na kwa madhumuni ya udhibiti wa forodha.

Ukiukaji wa masharti ya leseni ya uendeshaji.

44.-(1) Mwendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi anayekiuka masharti ya leseni, anaweza kutozwa faini, kusitishiwa au kufutiwa leseni ya uendeshaji au kufutiwa vivutio na Mamlaka.

(2) Mamlaka au mamlaka nyingine inaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya muendeshaji asiyezingatia masharti ya sheria.

*(d) Masharti yanayohusiana na uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje*

Maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje

45.-(1) Mtu anayekusudia kuzalisha bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje atafanya maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 8 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje yataambatanishwa na-
(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili cha kampuni mpya;
(b) mpango wa biashara unaolenga mauzo ya nje unaojumuisha taarifa zifuatazo:
(i) aina ya bidhaa inayokusudiwa kuzalishwa na masoko yanayotarajiwa;
(ii) utambuzi wa eneo la uzalishaji kwa mauzo ya nje;
(iii) aina na chanzo cha malighafi zitakazotumika katika uzalishaji;
(iv) masoko tarajiwa, thamani ya mauzo ya nje kwa mwaka, na

ajira zinazotarajiwa kuzalishwa;
(v) cheti cha tathmini ya athari za kimazingira; na
(vi) uthibitisho wa mtaji au uwezo wa kifedha wa kutekeleza uzalishaji;
(c) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje; na
(d) taarifa nyingine yoyote kadri Mamlaka inavyoweza kuhitaji.

Utoaji wa leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje

46. (1) Mamlaka inaweza, baada ya kujiridhisha kuwa mwombaji amekidhi masharti yaliyoainishwa katika Kanuni hizi, kutoa leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje kwa mwombaji kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 13 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje atahakikisha kwamba thamani ya mauzo ya nje ya kila mwaka ni zaidi ya Shilingi za Tanzania zenye thamani sawa na dola za Marekani laki moja.

(3) Leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje itakuwa halali kwa muda wa mwaka mmoja na inaweza kuhuishwa ndani ya miezi mitatu kabla ya ukomo.

(4) Maombi ya kuhuisha leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa kupitia Fomu Na. 10 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Uwasilisha wa taarifa ya robo mwaka

47. Mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje atawasilisha taarifa ya shughuli zake kila robo mwaka na kila mwaka kwa Mamlaka ikijumuisha masuala yafuatayo:
(a) malighafi zote zilizopokelewa na kutumika kwa ajili ya uzalishaji au usindikaji katika robo mwaka au mwaka uliopita;

(b) uzalishaji wa bidhaa zilizokamilishwa na zilizomalizika ikijumuisha bidhaa zinazopakiwa katika eneo la forodha na kusafirishwa nje ya nchi;
(c) mabaki ya taka na namna ya uondoshaji wake;
(d) hasara inayotokana na uvukizi, kumwagika, kuvuja au sababu nyinginezo;
(e) kiasi cha malighafi kilichosalia na bidhaa ambazo hazijakamilika ikiwa ni pamoja na bidhaa za ziada zilizohifadhiwa katika eneo la utengenezaji au usafirishaji katika kipindi cha robo mwaka;
(f) kiasi cha bidhaa zilizosafirishwa nje ya nchi katika robo mwaka na mwaka husika; na
(g) taarifa nyingine yoyote kadri itakavyohitajika na Mamlaka.

Wajibu wa kutunza na kutoa taarifa

48.-(1) Mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje anapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa na takwimu kama inavyotakiwa na Sheria, kanuni au sheria zote za nchi.

(2) Mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje ataweka katika eneo lake la biashara nyaraka zifuatazo:
(a) rejesta inayoainisha kiasi na maelezo ya malighafi zinazotumika kutengeneza bidhaa, kiasi na maelezo ya bidhaa zilizokamilika na zilizomalizika na namna ya uondoshaji wake;
(b) rejesta ya kuhifadhi taarifa za taka zinazotokana na uzalishaji wa bidhaa;
(c) vitabu vya hesabu, ankara, kibali cha forodha na hati zingine zinazohusiana na shughuli za uzalishaji; na

(d) kumbukumbu ya kiasi cha bidhaa zilizopotea kutokana na uvukizi, kumwagika, kuvuja au sababu nyinginezo.

(3) Mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje atawasilisha kwa Mamlaka vitabu vya hesabu, kumbukumbu na nyaraka zitakazohitajika kwa ajili ya ukaguzi wa afisa wa Mamlaka, na atamruhusu afisa kutengeneza dondoo kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

### *(e) Masharti yanayohusiana na uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani*

Maombi ya leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

49.-(1) Mtu anayekusudia kufanya uzalishaji na uchakataji wa bidhaa au huduma kwa ajili ya mauzo katika soko la ndani atafanya maombi ya leseni kupitia Fomu Na. 8 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya leseni ya uzalishaji au utoaji wa huduma kwa ajili ya soko la ndani yataambatishwa na-

(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni;

(b) uthibitisho kwamba kampuni inayoomba leseni haijawahi kufanya uzalishaji katika soko la ndani;

(c) nakala iliyothibitishwa ya katiba ya kampuni ;

(d) nakala ya namba ya mlipa kodi;

(e) mpango wa biashara unaoainisha aina ya uzalishaji au uchakataji au uunganishaji wa mashine au vifaa, aina ya malighafi zitakazotumika na bidhaa zitakazotengenezwa ili kuuzwa katika soko la ndani;

(f) uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutekeleza mradi;

(g) idadi ya wafanyakazi na uraia wao;

(h) jina na anuani ya wamiliki wa kampuni, wakurugenzi na katibu wa kampuni;
(i) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;
(j) uthibitisho wa usimikaji wa chombo, shughuli zitakazofanyika na taka zitakazozalishwa zinaendana na viwango vya kimazingira, usalama mahali pa kazi pamoja na sheria za usalama; na
(k) taarifa nyingine yoyote kadri itakavyohitajika na Mamlaka.

Ukaguzi wa eneo la uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

50.-(1) Mamlaka baada ya kupokea maombi itatembelea eneo la mradi ili kujiridhisha na taarifa zilizowasilishwa na mwombaji.

(2) Endapo Mamlaka itabaini kwamba maombi yaliyowasilishwa yana mapungufu itamjulisha mwombaji ya siku kumi na nne.

(3) Mwombaji baada ya kupokea taarifa ya mapungufu, atafanyia kazi kwa kurekebisha mapungufu na kuwasilisha tena maombi yake.

(4) Mamlaka inaweza, wakati wa uchakataji wa maombi, kumtaka mwombaji kuwasilisha taarifa za ziada kadri itakavyoona inafaa.

Leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

51.-(1) Mamlaka, baada ya kujiridhisha kwamba maombi yamezingatia masharti, itatoa leseni ya uzalishaji au utoaji wa huduma kwa ajili ya soko la ndani, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea maombi kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 13 katika Jedwali la Kwanza.

(2) Leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani itakuwa halali kwa muda wa miaka miwili.

(3) Leseni ya uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani inaweza kuhuishwa kupitia Fomu Na.10 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Haki na wajibu wa mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

52.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria, mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani atakuwa na haki, wajibu na atazingatia masharti yafuatayo:

(a) kupata vivutio vilivyoainishwa katika Sheria na Kanuni hizi;
(b) kuingiza bidhaa zake katika soko la ndani kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na sheria zote za nchi;
(c) huduma zinazotolewa na mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani zitatozwa kodi kwa mujibu wa sheria;
(d) mzalishaji kwa ajili soko la ndani atauza au atahamisha leseni yake baada ya kupata idhini ya Mamlaka;
(e) kuzalisha kwa kuzingatia mpango wake wa biashara;
(f) kuhakikisha uwepo au upatikanaji wa miundombinu ya kuhifadhi, kufungasha, uwekaji alama, upimaji na uchukuaji wa idadi ya bidhaa kila inapohitajika na Mamlaka;
(g) kutoa mafunzo ya utendaji kazi kwa wafanyakazi;
(h) kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya kila robo mwaka;
(i) kuzingatia sheria zinazosimamia masuala ya ajira, usalama mahali pa kazi, uhamiaji na mazingira;
(j) kupata kibali cha ujenzi kutoka kwa Mamlaka iwapo kuna ujenzi au marekebisho ya mindombinu; na
(k) kutokujihusisha katika shughuli yoyote isiyo halali nchini Tanzania.

Hatua dhidi ya ukiukaji wa masharti ya leseni ya uzalishaji

53.-(1) Mamlaka itachukua hatua dhidi ya mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani anayekiuka masharti ya leseni kama ifuatavyo:

(a) kusitisha vivutio;
(b) kufuta au kusitisha leseni; au
(c) kuvunja mkataba wa upangishaji katika eneo maalumu la kiuchumi.

Notisi ya kutotekeleza masharti ya leseni

54.-(1) Mamlaka itatoa notisi ya kutotekeleza masharti ya leseni kwa mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani na mzalishaji atatakiwa kujibu notisi hiyo ndani ya siku kumi na nne.

(2) Mamlaka baada ya kupokea majibu ya mzalishaji inaweza kuchukua hatua yoyote iliyoainishwa katika kanuni ya 53.

(3) Bila kuathiri kifungu cha 17(2) cha Sheria, mazingira mengine yanayoweza kupelekea ufutaji wa leseni ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya ndani yanajumuisha:

(a) mzalishaji kusitisha shughuli za uzalishaji kwa kipindi cha siku tisini mfululizo bila kutoa taarifa kwa Mamlaka au kuomba muda wa nyongeza kutoka kwa Mamlaka;
(b) kutozingatia masharti ya vivutio na leseni; au
(c) mzalishaji ametangazwa kuwa muflisi au amefilisika.

*(f) Masharti yanayohusiana na watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi*

Maombi ya kibali cha kutoa huduma

55.-(1) Mtu anayekusudia kutoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi atafanya maombi ya kibali kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 14 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi hayo yataambatishwa na:

(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni;
(b) namba ya mlipa kodi na namba ya usajili ya kodi ya ongezeko la thamani;
(c) nakala iliyothibitishwa ya katiba ya kampuni;

(d) leseni ya biashara;
(e) mpango wa biashara unaoainisha aina ya huduma itakayotolewa katika eneo maalumu la kiuchumi;
(f) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi;
(g) uthibitisho wa uzoefu wa utoaji huduma inayopendekezwa kutolewa katika eneo maalumu la kiuchumi;
(h) uthibitisho wa uwezo wa kifedha wa kutoa huduma husika; na
(i) taarifa nyingine kadri Mamlaka itakavyoona inafaa.

Kibali cha mtoa huduma

56.-(1) Mamlaka, baada ya kujiridhisha na maombi, inaweza kutoa kibali cha utoaji huduma kwa mwombaji kama kilivyoainishwa katika Fomu Na. 15 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kibali cha kutoa huduma kitakuwa halali kwa muda wa miaka miwili na kinaweza kuhuishwa kila mwaka.

(3) Mtoa huduma anaweza kufanya maombi ya uhuishaji wa kibali cha mtoa huduma kupitia Fomu Na. 14 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Mtoa huduma kutostahili kupata vivutio

57. Mtoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi hatakuwa na haki ya kupata vivutio vya kikodi.

Mamlaka ya kutoza kodi ya pango

58. Mamlaka inaweza kutoza kodi ya pango, ada au tozo katika eneo maalumu la kiuchumi.

## SEHEMU YA SITA
## VIVUTIO VYA UWEKEZAJI KATIKA ENEO MAALUMU LA KIUCHUMI

Vivutio vya mwendelezaji

59. Mwendelezaji wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kupata vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine yoyote inayotozwa kwenye bidhaa za mtaji katika uendelezaji;
(b) msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;
(c) msamaha wa kodi ya zuio kwenye gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;
(d) msamaha wa kodi ya zuio kwenye riba katika mikopo kutoka nje ya nchi;
(e) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine inayopaswa kulipwa wakati wa uingizaji wa gari moja kwa ajili ya huduma za utawala, magari ya kubebea wagonjwa, magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili kwa ajili ya usafirishaji wa wafanyakazi kuelekea na kutoka katika eneo maalumu la kiuchumi;
(f) viza ya biashara wakati wa kuingia nchini kwa wafanyakazi kwa muda usiozidi miezi miwili;
(g) msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za maji, umeme, gesi na simu;
(h) msamaha wa tozo za bandari;
(i) vivutio visivyo vya kikodi kulingana na uwekezaji kwa kuzingatia makubaliano baina ya mwekezaji na Serikali;
(j) msamaha wa ushuru wa stempu kwenye nyaraka zozote zinazohusiana na uhamishaji, ukodishaji au uwekaji dhamana wa mali inayohamishika au

isiyohamishika iliyopo katika eneo maalumu la kiuchumi; na

(k) msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya ujenzi na huduma za ujenzi.

Vivutio vya mwendeshaji

60. Mwendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi anaweza kupata vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;

(b) msamaha wa kodi ya zuio kwenye pango, gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(c) msamaha wa kodi ya zuio kwenye riba katika mikopo kutoka taasisi za kifedha za nje ya nchi;

(d) msamaha wa kodi, ada na tozo zinazotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika eneo maalumu la kiuchumi kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;

(e) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine inayopaswa kulipwa wakati wa uingizaji wa gari moja kwa ajili ya huduma za utawala, magari ya kubebea wagonjwa, magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili kwa ajili ya usafirishaji wa wafanyakazi kuelekea na kutoka katika eneo maalumu la kiuchumi;

(f) viza ya biashara wakati wa kuingia nchini kwa wafanyakazi kwa muda usiozidi miezi miwili;

(g) msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za maji, umeme, gesi na simu;

(h) msamaha wa tozo za bandari;

(i) msamaha wa ushuru wa stempu kwenye nyaraka zozote zinazohusiana na uhamishaji, ukodishaji au uwekaji dhamana wa mali inayohamishika au isiyohamishika iliyo katika eneo maalumu la kiuchumi; na

(j) vivutio visivyo vya kikodi kulingana na uwekezaji kwa kuzingatia makubaliano baina ya mwekezaji na Serikali.

Vivutio vya mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

61. Mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani anaweza kupata vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine yoyote inayotozwa kwenye mali ghafi na bidhaa za mtaji katika uzalishaji;

(b) msamaha wa kodi ya zuio kwenye pango, gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(c) msamaha wa kodi ya zuio kwenye riba katika mikopo kutoka taasisi za kifedha nje ya nchi;

(d) msamaha wa kodi, ada na tozo zinazotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika eneo maalumu la kiuchumi kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;

(e) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine inayopaswa kulipwa wakati wa uingizaji wa gari moja kwa ajili ya huduma za utawala, magari ya kubebea wagonjwa, magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili kwa ajili ya usafirishaji wa wafanyakazi kuelekea na kutoka katika eneo maalumu la kiuchumi;

(f) viza ya biashara wakati wa kuingia nchini kwa wafanyakazi kwa muda usiozidi miezi miwili;
(g) msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za maji, umeme, gesi na simu;
(h) vivutio visivyo vya kikodi kulingana na uwekezaji kwa kuzingatia makubaliano baina ya mwekezaji na Serikali;
(i) msamaha wa tozo za bandari; na
(j) msamaha wa ushuru wa stempu kwenye nyaraka zozote zinazohusiana na uhamishaji, ukodishaji au uwekaji dhamana wa mali inayohamishika au isiyohamishika iliyo katika eneo maalumu la kiuchumi.

Masharti ya utoaji vivutio kwa mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani

62.-(1) Mzalishaji kwa ajili ya soko la ndani anaweza kupewa vivutio vya uwekezaji vilivyoainishwa katika kanuni ya 64, iwapo uwekezaji wake umejikita katika kiwanda au sekta zifuatazo:
(a) viwanda vya kuzalisha madawa na vifaa tiba;
(b) viwanda vya kuunganisha na kuzalisha bidhaa za gari, boti, mitambo au vipuri vya mitambo na magari;
(c) uwekezaji katika miradi ya uhifadhi wa mazingira hususani uwekezaji kwenye mifumo au teknolojia ya uteketezaji wa taka ngumu, hatarishi na za hospitali; na
(d) sekta nyingine itakayopendekezwa na Mamlaka na kuidhinishwa na Waziri.

Vivutio vya mzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje

63. Mzalishaji katika eneo maalumu la uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje anaweza kupata vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine yoyote inayotozwa kwenye mali ghafi na bidhaa za mtaji katika uzalishaji;

(b) msamaha wa kodi ya mapato ya kampuni kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;

(c) msamaha wa kodi ya zuio kwenye pango, gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(d) msamaha wa kodi ya zuio kwenye riba katika mikopo kutoka taasisi za kifedha nje ya nchi;

(e) msamaha wa kodi, ada na tozo zinazotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika maeneo maalumu ya kiuchumi kwa kipindi cha miaka kumi ya mwanzo;

(f) msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine inayopaswa kulipwa wakati wa uingizaji wa gari moja kwa ajili ya huduma za utawala, magari ya kubebea wagonjwa, magari ya zimamoto na mabasi yasiyozidi mawili kwa ajili ya usafirishaji wa wafanyakazi kuelekea na kutoka katika maeneo maalumu ya kiuchumi;

(g) viza ya biashara wakati wa kuingia nchini kwa wafanyakazi kwa muda usiozidi miezi miwili;

(h) msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za maji, umeme, gesi na simu;

(i) vivutio visivyo vya kikodi kulingana na uwekezaji kwa kuzingatia makubaliano baina ya mwekezaji na Serikali;

(j) msamaha wa tozo za bandari; au
(k) msamaha wa ushuru wa stempu kwenye nyaraka zozote zinazohusiana na uhamishaji, ukodishaji au uwekaji dhamana wa mali inayohamishika au isiyohamishika iliyo katika eneo maalumu la kiuchumi.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI YA KUJITOA AU KUBADILISHA SHUGHULI YA UZALISHAJI KATIKA ENEO MAALUMU LA KIUCHUMI

Kubadilisha shughuli ya uzalishaji

64.-(1) Mmiliki wa leseni anaweza kufanya maombi kwa Mamlaka ya kujitoa, kuhama eneo maalumu la uchumi au kubadili shughuli ya uzalishaji kwa mauzo ya nje kuwa uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani.

(2) Endapo Mamlaka itapokea maombi kwa mujibu wa kanuni hii na kabla ya kutoa kibali kwa mwombaji kujitoa, ama kuhama itajiridhisha na masuala yafuatayo:
(a) mwombaji kuwasilisha uthibitisho wa malipo ya deni lolote analodaiwa na Mamlaka au watoa huduma katika eneo maalumu la kiuchumi;
(b) kuwa mwombaji hajauza ama kuhamisha umiliki wa biashara yake kwa kampuni nyingine bila kibali cha Mamlaka; na
(c) ulipaji wa kodi stahiki zitakazo tozwa wakati wa kubadili aina ya shughuli inayofanywa katika eneo maalumu la kiuchumi, au wakati wa kujitoa.

(3) Mamlaka itatoa notisi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya taratibu za mwombaji kufanyiwa makadirio ya kodi kwa lengo la kurejesha kodi alizosamehewa.

(4) Baada ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kufanya tathmini na baada ya mwombaji kukamilisha masuala yote ya kikodi, Kamishna atatoa uthibitisho wa maandishi wa ukamilishaji wa masharti ya kiforodha na kuwasilisha kwa Mamlaka.

(5) Mamlaka itatoa idhini ya kujitoa au kuhama eneo maalumu la kiuchumi kwa mwombaji iwapo itapokea uthibitisho wa maandishi wa ukamilishaji wa masharti ya kiforodha kutoka kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(6) Mwendeshaji wa eneo maaalumu la kiuchumi atahakikisha kuwa mwekezaji aliyesajiliwa kwenye eneo analoliendesha wanazingatia masharti ya kujitoa kwenye eneo maalumu la kiuchumi.

Haki ya Mamlaka kununua au kutonunua majengo

65.-(1) Mamlaka itakuwa na haki ya kwanza ya kukubali au kukataa kununua jengo la mwekezaji anayejitoa au kuhama eneo maalumu la kiuchumi.

(2) Mamlaka ikiridhia itamlipa mwekezaji fidia ya gharama za ujenzi kwa thamani itakayobainishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali baada ya uthamini wa jengo kufanyika.

(3) Mamlaka inaweza kukubali kuchukua jengo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) kwa lengo la kumpatia mwekezaji mwingine ambaye atakuwa tayari kulipa fidia iliyobainishwa.

Mamlaka kusimamia uuzaji wa majengo

66. Mamlaka itakuwa na wajibu wa kusimamia uuzaji wa majengo yaliyojengwa na wawekezaji ndani ya eneo maalumu la kiuchumi.

Uzingatiaji wa sheria katika uuzaji wa majengo

67. Uuzaji wa majengo katika eneo maalumu ya kiuchumi utazingatia taratibu na sheria zote za nchi.

## SEHEMU YA NANE

## MASHARTI YA JUMLA

Ufutaji au usitishaji wa leseni au kibali

68.-(1) Mamlaka inaweza kufuta cheti, leseni au kibali kilichotolewa chini ya Kanuni hizi iwapo itaridhika kwamba-

(a) cheti au leseni ilipatikana kwa njia ya udanganyifu au kwa kutoa taarifa za uongo;
(b) cheti au leseni imerekebishwa au kuhamishwa kwa mtu au uwekezaji mwingine bila idhini ya Mamlaka;
(c) mwekezaji ameshindwa kutimiza wajibu ulioainishwa chini ya Sheria na Kanuni hizi;
(d) mwekezaji hajaanza kutekeleza mradi ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia kutolewa kwa cheti au leseni bila sababu ya msingi; au
(e) mwekezaji hajawasilisha taarifa za utekelezaji na maendeleo ya mradi wa uwekezaji kwa miezi ishirini na nne mfululizo.

Zuio la kuongeza msamaha wa kodi

69. Endapo muda wa leseni umehuishwa au kuongezwa, uhuishaji huo au nyongeza hiyo haitaongeza muda wa msamaha wa kodi uliotolewa awali kwa mwekezaji.

Zuio dhidi ya kufanya shughuli zisizo na leseni

70. Mmiliki wa leseni anapaswa kufanya biashara iliyoainishwa katika leseni aliyopewa na Mamlaka.

Mamlaka kuamua aina ya bidhaa zitakazozalishwa

71.-(1) Mamlaka itaamua bidhaa zitakazozalishwa na aina ya huduma zitakazotolewa katika eneo maalumu la kiuchumi.

(2) Bidhaa zifuatazo haziruhusiwi kuzalishwa, au kuhifadhiwa katika eneo maalumu kiuchumi:

Sura ya 223

(a) silaha au risasi, au vifaa vingine vya kivita kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi;

(b) milipuko na vitu vingine hatarishi;
(c) madawa ya kulevya; na
(d) bidhaa nyingine zilizokatazwa kwa mujibu wa sheria.

Zuio la kuingia au kufanya shughuli kwenye eneo maalumu la uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje

72.-(1) Mtu hataruhusiwa kuingia au kufanya shughuli yoyote katika eneo maalumu la kiuchumi bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa Mamlaka.

(2) Masharti ya kanuni hii hayatatumika kwa-
(a) maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama katika utekelezaji wa majukumu yao;
(b) afisa aliyeidhinishwa kuingia katika eneo maalumu la kiuchumi; au
(c) mtu yeyote aliyeajiriwa na mwendelezaji, mwendeshaji, mzalishaji au mtoa huduma aliyeidhinishwa na sheria kutoa huduma za kijamii katika utekelezaji wa majukumu yao.

Usimamizi wa mazingira

73. Mamlaka, kwa kushirikiana na mamlaka yenye dhamana na usimamizi wa mazingira, itatekeleza yafuatayo katika maeneo maalumu ya kiuchumi:
(a) kuweka mipango ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira , rasilimali za asili, na bayoanuwai;
(b) kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira;
(c) kuweka utaratibu wa hatua madhubuti za uondosjaji taka ngumu na taka miminika ikiwa ni pamoja na kusimamia viwango bora vya mazingira;
(d) kufanya tathmini za haraka za athari za kimazingira;
(e) kuweka mbinu za kisasa za utekelezaji na ufuatiliaji wa mazingira, ikiwa ni

pamoja na taratibu za uzingatiaji wa sheria na ufuatiliaji;
(f) kuhakikisha uondoshaji wa taka, kemikali zinazotokana na shughuli za viwanda na usindikaji unafanyika kwa utaratibu; na
(g) kuanzisha maeneo maalumu ya kiuchumi kwa lengo la kuhamasisha uchumi wa kijani pale inapofaa.

Mwongozo wa Usanifu wa ujenzi wa miundombinu

74.-(1) Mamlaka kwa kushirikiana na mamlaka husika, itaandaa Mwongozo wa Usanifu na Ujenzi wa miundombinu ya eneo maalumu la kiuchumi.

(2) Mwendelezaji au mwendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi anayekusudia kufanya ujenzi, upanuzi au marekebisho ya miundombinu atazingatia taratibu na viwango vilivyoainishwa kwenye Kanuni hizi na Mwongozo wa Usanifu na Ujenzi ulioandaliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

(3) Bila kuathiri masharti ya utoaji wa leseni ya uendelezaji au uendeshaji wa eneo maalumu la kiuchumi, mmiliki wa leseni asiyezingatia Mwongozo wa Usanifu na Ujenzi anatenda kosa.

(4) Mamlaka inaweza kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutoa notisi ya kuzingatia Mwongozo wa Usanifu na Ujenzi, kusimamisha ujenzi au kufuta leseni ikibaini kuwa mwendelezaji au mwendeshaji amekiuka masharti ya Mwongozo.

Notisi ya kurekebisha wa miundombinu

75.-(1) Mamlaka itatoa Notisi inayobainisha muda wa kurekebisha miundombinu kwa mmiliki wa leseni iwapo miundombinu katika eneo maalumu la kiuchumi itakuwa katika hali ya uharibifu au itapata hitilafu ya kiufundi au kushindwa kufanya kazi ipasavyo na kuathiri shughuli za uzalishaji katika eneo maalumu.

(2) Mmiliki wa leseni ambaye hatazingatia masharti ya notisi iliyotolewa anatenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni hamsini.

Ada na tozo

76. Ada za maombi, tozo au malipo yoyote yanayotakiwa kulipwa kwa Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni hizi yatalipwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Usiri wa taarifa

77. Mamlaka itachukulia tarifa zote zinazowasilishwa na wawekezaji kuwa ni siri na haitatoa tarifa hizo kwa mtu isipokuwa kwa matakwa ya sheria.

Rufaa

78.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka kuhusu-

(a) kukataliwa kupewa cheti au leseni chini ya Kanuni hizi;
(b) kukataliwa kupewa vivutio kwa ajili ya ukarabati au upanuzi wa mradi;
(c) kukataliwa kuongezewa muda wa uhai wa cheti au leseni; au
(d) kufutiwa cheti au leseni,

anaweza kukata rufaa kwa Waziri kwa kuandika barua ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe aliyopokea uamuzi huo.

(2) Baada ya kupokea rufaa, Waziri anaweza ndani ya siku thelathini kuthibitisha, kufuta, kurekebisha, au kutoa maelekezo mahsusi kuhusu uamuzi uliotolewa na Mamlaka.

(3) Uamuzi wa Waziri utakaotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) utakuwa wa mwisho.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (3), mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri chini ya kanuni ndogo ya (2) anaweza kufanya maombi ya marejeo.

Mapitio

79.-(1) Mwekezaji ambaye hajaridhika na uamuzi wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya

Uwekezaji kuhusu uidhinishaji wa vivutio au suala lingine lililowasilishwa chini ya kanuni ya 8 anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa kuandika barua kwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji akianisha sababu za mapitio hayo ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya kupokea uamuzi.

(2) Maombi ya mapitio kwenda Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji yatawasilishwa kwa Katibu wa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji.

(3) Baada ya kupokea maombi hayo, Kamati itapitia na kutoa uamuzi, na uamuzi huo utakuwa wa mwisho.

Ushughulikiaji wa malalamiko

80.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 38 cha Sheria, mwekezaji ambaye hakuridhishwa na mwenendo, tabia, kitendo au uamuzi wa taasisi ya Serikali kuhusu masuala ya uwekezaji, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka kwa njia ya maandishi au kupitia mfumo unganishi wa kielektroniki au anwani ya posta ya Mamlaka.

(2) Baada ya kupokea malalamiko, Mamlaka itapaswa, ndani ya siku thelathini (30), kuitisha kikao au vikao kadiri itakavyohitajika baina ya mwekezaji na taasisi inayolalamikiwa kwa ajili ya kusikilizwa na kupata utatuzi wa malalamiko hayo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 38(2) cha Sheria, Mamlaka inaweza, wakati wa kuchunguza na kutathmini malalamiko, kuwataka wahusika kuwasilisha nyaraka au vielelezo vyovyote vinavyohusika kwa ajili ya utatuzi wa malalamiko husika.

(4) Baada ya kuchunguza na kutathmini malalamiko ya mwekezaji chini ya kanuni ndogo ya (3), Mamlaka itatoa uamuzi wake kwa njia ya maandishi na kuwasilisha uamuzi huo kwa wahusika kupitia mfumo unganishi wa kielektroniki au anwani za posta za wahusika.

(5) Endapo Mamlaka itashindwa kushughulikia malalamiko ndani ya siku thelathini au mlalamikaji hakuridhishwa na uamuzi wa Mamlaka au namna ambavyo Mamlaka imeshughulikia malalamiko hayo, mlalamikaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa Waziri.

(6) Baada ya kupokea malalamiko ya mwekezaji Waziri anaweza ndani ya siku kumi na nne kuthibitisha, kubadilisha au kutoa maelekezo mahsusi kuhusu uamuzi uliotolewa na Mamlaka.

(7) Mwekezaji ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri chini ya kanuni ndogo ya (6) anaweza kuendelea na taratibu nyingine za kisheria za utatuzi wa malalamiko yake.

(8) Mamlaka itatunza na kuhuisha kanzidata yenye kumbukumbu za malalamiko yaliyopokelewa na kushughulikiwa na Mamlaka.

Uharibifu wa mali

81. Mtu ambaye kwa makusudi au kwa uzembe ataharibu mali ya mwekezaji na kusababisha upotevu wa fedha anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni kumi na malipo ya fidia inayohusiana na uharibifu huo.

Kufutwa kwa Kanuni
TS. Na
6 la 2003
359 la 2012
501 la 2023

82. Kanuni za Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo ya Nje, Kanuni za Maeneo Maalumu ya Uwekezaji na Kanuni za Uwekezaji Tanzania. zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

FOMU Na. 1

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

FOMU YA MAOMBI YA HADHI YA UWEKEZAJI WA KIMKAKATI

**1.** Mimi/ Sisi Mkurugenzi/ Wakala wa……………………………………………………………

**2.** Taja Jina la Kampuni au Taasisi ya Kibiashara na mahali ilipo ofisi iliyosajiliwa
………………………………………………………………………………………………

**3.** Ambatisha nakala za nyaraka zifuatazo:
(a) katiba ya Kampuni;
(b) cheti cha usajili wa kampuni;
(c) nakala ya andiko la mradi au utafiti unaoonesha muda wa utekelezaji; programu ya utekelezaji na muda wa kuanza uendeshaji; na
(d) ushahidi wa ufadhili wa kifedha na umiliki wa ardhi ya mradi

**4.** Jina la eneo mradi ulipo
…………………………………………………………………………….

**5.** Orodhesha Maafisa Wakuu wa Kampuni/Taasisi ya kibiashara
(a) ……………………………………………………………………..
(b) ……………………………………………………………………..
(c) ……………………………………………………………………..

**6.** Idadi ya hisa za mtaji za kampuni zilizoidhinishwa
………………………………………………………………………………………………

**7.** Kiasi cha mtaji unaokusudiwa kuwekezwa katika mradi
………………………………………………………………………………………………

**8.** Ambatisha risiti ya malipo ya fedha taslimu kuthibitisha malipo ya ada ya usajili ambayo haitarejeshwa.

**9.** Tamko

Mimi…………………………………………………wa
S.L.P………………………………………
Naapa/ Nathibitisha na kutamka kwa dhati kwamba kwa wadhifa wangu kama Mkurugenzi/ au wakala aliyeidhinishwa nimezingatia matakwa ya Sheria ya Uwekezaji

na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Sheria Na. 6 ya mwaka 2025, kuhusu masuala ya usajili Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Imetolewa hapa……………….……….... (Mkoa)}

Na ……………………………………..… (Mwombaji)

Leo…………siku ya……Mwezi……. Mwaka……..…}

Mbele yangu:

Jina:…………………………………………………..
Saini:……………………….…………………………
Tarehe: ……………………………………………….
Wadhifa: Kamishna wa viapo

Jaza panapohusika tu, vinginevyo onesha "N/A"

MAOMBI KWA UFUPI NA MAELEZO YA ZIADA

**10.** Jina la taasisi ya kibiashara: ………………………………………...

**11.** Aina ya usajili wa biashara………………………………………….

**12.** Namba ya Usajili wa biashara……………

**13.** Tarehe ya Usajili wa Biashara……
S.L.P: …………………..
Mji: …………………….

**14.** Sekta……………………Sekta ndogo…………………….
**15.** Mpango wa ufadhili wa uwekezaji kwa Dola/TShs

| | |
|---|---|
| Mtaji wa Mwekezaji kutoka Nje …………………….. | Mtaji wa Mwekezaji kutoka Ndani …………………….. |
| Mtaji wa Mkopo kutoka Nje …………………….. | Mtaji wa Mkopo kutoka Nchini …………………….. |

**16.** Malengo ya Mradi:…………………………………………………………………...................

**17.** Mradi unavyohusiana na mipango ya Maendeleo yaNchi…………………...........
**18.** Uwezo wa mradi wa Kuzalisha utakapokamilika:………………………….........
**19.** Aina ya Teknolojia mpy itakayotumika………………………………….........

**20.** Makisio ya fedha za kigeni zitakazozalishwa wakati mradi utakapokamilika…………………………………………………….............

**21.** Ajira:

(a) Watanzania…………….wageni……………………jumla…………….

(b) Ajira za moja kwa moja…………… vibarua………….zisizo za moja kwa moja…………….. Jumla…………………

**22.** Makisio ya mapato ya Serikali yatakayopatikana mradi utakapokamilika

(a) Mapato ya kodi ya moja kwa moja kwa mwaka…………………………….
(b) Kodi zisizo za moja kwa moja ………………………………………….

**23.** Muda wa utekelezaji wa mradi……………….

**24.** Mahali ulipo mradi

(a) Kiwanja Na……….Kitalu Na……………..

(b) Mtaa…………………Wilaya………………….Mkoa…………………
(Ambatisha ramani kuonesha eneo mradi ulipo)

(c) Ukubwa wa Ardhi kwa ajili ya mradi (ekari)…………………………………

(d) Hali ya umiliki wa Ardhi…………………………………………………...

**25.** Iwapo mradi umeshaanza utekelezaji au ni upanuzi, elezea yafuatayo;

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Mtaji uliowekezwa hadi sasa (Dola Za Marekani/Shs) | ……………………………… |
| (b) | Asilimia ya Mradi uliokamilika/ au asilimia ya ardhi iliyoendelezwa | ……………………………… |
| (c) | Taarifa ya miundombinu na vifaa vilivyopo eneo la mradi | ……………………………… |
| (d) | Ajira za moja kwa moja zilizopo | ……………………………… |
| (e) | Idadi ya vibarua waliopo | ……………………………… |
| (f) | Makisio ya ajira za moja kwa moja zilizopo | ……………………………… |
| (g) | Uwezo wa Uzalishaji uliopo | ……………………………… |
| (h) | Kodi za moja kwa moja zinazolipwa (TRA) | ……………………………… |
| (i) | Kodi zisizo za moja kwa moja zinazolipwa | ……………………………… |
| (j) | Changamoto zinazokabili mradi | ……………………………… |

| Majina ya Wanahisa | Uraia | % ya Umiliki |
|---|---|---|
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |

| Mchanganuo wa Gharama za Uwekezaji | Tshs |
|---|---|
| (a) Ardhi/Majengo | ……………………… |
| (b) Mitambo | ……………………… |
| (c) Magari | ……………………… |
| (d) Samani & Vifaa | ……………………… |
| (e) Gharama za awali | ……………………… |
| (f) Mengineyo | ……………………… |
| (g) Mtaji wa kufanyia Kazi | ……………………… |
| Jumla | ……………………… |

Mawasiliano:
Jina………………………………………Cheo…………………………….
Simu…………………………………… Nukushi…………………………
Barua pepe…………………………….

Maombi ya vivutio vya ziada vya kikodi na visivyo vya Kikodi

| Na | Aina ya kivutio cha kikodi na ambacho si cha kikodi | Jina la Bidhaa/huduma | Kipimo cha bidhaa | Makisio ya kiasi cha bidhaa (ambatisha orodha ya HS Codes endapo itahitajika) | Makisio ya thamani ya bidhaa/ huduma | Makisio ya thamani ya msamaha wa kodi kwa kivutio husika | Muda wa Utekelezaji wa vivutio kwa kipindi (miaka) | Umuhimu wa kivutio |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Mfano Kodi ya Ongezeko la thamani | Vifaa vya ujenzi | Mbalimbali | Kiambatisho I kuhusu vifaa vya ujenzi | | | | |

Kiambatisho I -Orodha ya kina ya vifaa vya ujenzi vya Mradi

| Na: | Namba ya HS | Jina la Kifaa | Aina/ | Kundi la bidhaa | Kipimo cha Kifaa | Kiasi | Makisio ya gharama ya vifaa -CIF |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | Vifaa vya ujenzi | | | |
| 2. | | | | | | | |
| | | | | | | | Jumla |

FOMU Na. 2

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8)*

FOMU YA UWASILISHAJI WA MASUALA YA UWEKEZAJI KWA KAMATI YA MAENDELEO YA TAIFA YA UWEKEZAJI KWA MAAMUZI

1. Jina la Taasisi ya Kibiashara au Taasisi ya Serikali inayowasilisha masuala ya Uwekezaji yanayohitaji mwongozo wa Kamati ya Maendeleo ya Taifa ya Uwekezaji
…………………………………………………………………..

2. Andika masuala yanayohusu Uwekezaji/ masuala yanayohitaji kutatuliwa na Kamati ya Taifa ya maendeleo ya Uwekezaji
……………………………………………………………………..

3. Ambatisha nakala ya nyaraka zifuatazo katika wasilisho,

(a) Nakala ya Andiko linaloelezea suala husika kwa kina,

……………………………………………………………..

(b) Wizara, Sekta, Idara, au Mamlaka inayosimamia suala husika,
…………………………………………………………….
(c) Hatua inayopendekezwa kuchukuliwa na Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji

…………………………………………………………..

4. Tamko la Mwombaji

Mimi……………………………………. wa S.L.P……………………………
Naapa kwamba mimi hni Mkurugenzi/ Wakala alieidhinishwa

……………………………..
Mwombaji

5. Mawasiliano
Jina:……………………………Cheo:……………………………..

Simu:…………………………………        Nukushi:………………………..

Barua pepe:……………………………

WASILISHO KWA UFUPI

*Tangazo la Serikali Na. 466 (Linaendelea)*

| Na. | Maelezo ya Kina | Taasisi husika | Madhara kwa mazingira ya uwekezaji au Taasisi za Kibiashara | Hatua inayopaswa kuchukuliwa | Pendekezao kwa Kamati ya Taifa ya Maendeleo ya Uwekezaji kwa maamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

FOMU Na. 3

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 11 (1) )*

FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA UWEKEZAJI

**1.** Mimi/Sisi/…………………………….(Mkurugenzi/Wakurugenzi/Wamiliki tunaomba usajili wa Uwekezaji chini ya kifungu cha 15 cha Sheria na Kanuni za Uwekezaji za mwaka 2025

**2.** Kampuni/Jina la Biashara :………………………………………………….

**3.** Aina ya Usajili wa Biashara :………………….(nakala imeambatishwa)

**4.** Namba ya Uasjili wa Biashara:………………………..

**5.** Tarehe ya Usajili wa Biashara:……………

**6.** Namba ya Utambuzi ya Mlipa Kodi……………….(nakala imeambatishwa)

**7.** S.L.P: …………………………

**8.** Mji: ……………………………

**9.** Sekta: …………………… Sekta ndogo:……………………………………..

**10.** Aina ya Mradi/Shughuli:……………………………………………………………… ……

**11.** Jumla ya Mtaji uliowekezwa: ……..……………………………………………………..

**12.** Ufadhili wa mpango wa Uwekezaji kwa Milioni

| | |
|---|---|
| Mtaji wa Mwekezaji kutoka Nje<br>…………………….. | Mtaji wa Mwekezaji kutoka Ndani<br>…………………….. |
| Mtaji wa Mkopo kutoka Nje<br>…………………….. | Mtaji wa Mkopo kutoka Nchini<br>…………………….. |

**13.** Uwezo wa Uzalishaji:…………………………………………………………...

**14.** Taarifa za Ajira

(a) Watanzania…………….Wageni……………………Jumla…………………….

**15.** Muda wa utekelezaji wa mradi……………….

**16.** Mahali ulipo mradi

(a) Kiwanja Na…….Kitalu Na……………..

(b) Mtaa…………………Wilaya………………….Mkoa…………………
(Ambatisha ramani kuonesha eneo mradi ulipo)

(c) Ukubwa wa Ardhi kwa ajili ya mradi (ekari)…………………………………

(d) Hali ya umiliki wa Ardhi……………………………………………………

| **17.** Majina ya Wanahisa | Uraia | % ya Umiliki |
|---|---|---|
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |

**18.** Mawasiliano:

Jina……………………………………Cheo…………………………

Simu…………………………………  Nukushi…………………………

Barua pepe……………………………..

**19.** TAMKO:

Mimi………………………………………………wa
S.L.P………………………………………………….
Naapa/ Nathibitisha na kutamka kwa dhati kwamba kwa wadhifa wangu kama Mkurugenzi/ au wakala aliyeidhinishwa nimezingatia matakwa ya Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025, kuhusu masuala rejea ya usajili wa Taasisi ya Kibiashara chini ya Sheria hii.
Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Imetolewa hapa………….……….... (Mkoa)}

Na  ……………………………………..… (Mwombaji)

Leo…………siku ya……Mwezi……. Mwaka……..…}

Mbele yangu:

Jina:…………………………………………………..
Saini:……………………….…………………………
Tarehe: ……………………………………………….
Wadhifa: Kamishna wa viapo

FOMU Na. 4

(*Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 13 (1)* )

FOMU YA MAOMBI YA CHETI CHA UWEKEZAJI / KUHUISHA CHETI CHA UWEKEZAJI

**1.** Mimi/ Sisi Mkurugenzi/ Wakala wa………………………………………

**2.** Taja Jina la Kampuni au taasisi ya kibiashara na mahali ilipo ofisi iliyosajiliwa

……………………………………………………………………………

**3.** Ambatisha nakala za nyaraka zifuatazo:

(a) Katiba ya Kampuni;

(b) Cheti cha Usajili wa Kampuni ;

(c) Nakala ya Andiko la Mradi au utafiti unaonesha muda wa utekelezaji, programu ya utekelezaji na muda wa kuanza uendeshaji au andiko la mradi na sababu za msingi za kuhuisha cheti; na

(d) Ushahidi wa ufadhili wa kifedha na umiliki wa ardhi ya mradi

**4.** Jina la eneo mradi ulipo ……………………………………………………………….

**5.** Orodhesha Maafisa Wakuu wa Kampuni/Taasisi ya kibiashara

(a) ………………………………………………………………………….

(b) ………………………………………………………………………….

(c) ………………………………………………………………………….

**6.** Andika Hisa za mtaji za Kampuni zilizoidhinishwa ………………………………….

**7.** Andika Mtaji unaokusudiwa kuwekezwa katika mradi ……………………………..

**8.** Ambatisha Hundi/ risiti kwa fedha taslimu kuthibitisha malipo ya ada ya maombi ya cheti au uhuishaji wa cheti ambayo haitarejeshwa

**9.** Tamko

Mimi…………………………………………………wa
S.L.P…………………………………………………….
Naapa/ Nathibitisha na kutamka kwa dhati kwamba kwa wadhifa wangu kama Mkurugenzi/ au wakala aliyeidhinishwa nimezingatia matakwa ya Sheria ya Uwekezaji

na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025, kuhusu masuala rejea ya usajili wa Taasisi ya Kibiashara chini ya Sheria hii.
Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Imetolewa hapa………….………... (Mkoa)}

Na …………………………………..… (Mwombaji)

Leo…………siku ya……Mwezi……. Mwaka……..…}

Mbele yangu:

Jina:…………………………………………………..
Saini:……………………….…………………………
Tarehe: ……………………………………………….
Wadhifa: Kamishna wa viapo

Ambatisha pale panapohusika tu, vinginevyo onesha "N/A"

MAOMBI KWA UFUPI NA MAELEZO YA ZIADA

**10.** Jina la Taasisi ya Kibiashara: ………………………………………...

**11.** Aina ya Usajili wa Biashara………………………………………

**12.** Namba ya Usajili wa Biashara……………Tarehe ya Usajili wa Biashara………….

S.L.P: ……………
Mji: ………………

**13.** Sekta……………………Sekta ndogo…………………

**14.** Mpango wa ufadhili wa Uwekezaji kwa Milioni za US$/TShs

| | |
|---|---|
| Mtaji wa Mwekezaji kutoka Nje | Mtaji wa Mwekezaji kutoka Ndani |
| …………………….. | …………………….. |
| Mtaji wa Mkopo kutoka Nje | Mtaji wa Mkopo kutoka Nchini |
| …………………….. | …………………….. |

**15.** Malengo ya Mradi:……………………………………………………………

**16.** Uwezo wa mradi wa Kuzalisha utakapokamilika: …………………………..

**17.** Ajira:

(a) Watanzania……………..Wageni……………………Jumla…………….

(b) Ajira za Moja kwa Moja…………… Vibarua………………….
Zisizo za Moja kwa Moja…………….. Jumla………………….

**18.** Makisio ya mapato ya Serikali yatakayopatikana mradi utakapokamilika

(c) Mapato ya kodi ya moja kwa moja kwa mwaka……………………………...
(d) Kodi zisizo za moja kwa moja ………………………………………………….

**19.** Muda wa utekelezaji wa mradi……………….

**20.** Mahali ulipo mradi

(a) Kiwanja Na………Kitalu Na…………

(b) Mtaa…………………Wilaya…………………. Mkoa…………………
(Ambatisha ramani kuonesha eneo mradi ulipo)

| Majina ya Wanahisa | Uraia | % ya Umiliki |
|---|---|---|
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |
| …………………….. | …………………….. | …………………….. |

| Mchanganuo wa Gharama za Uwekezaji | Dola za Marekani/ Shs. |
|---|---|
| (a) Ardhi/Majengo | ……………………… |
| (b) Mitambo | ……………………… |
| (c) Magari | ……………………… |
| (d) Samani & Vifaa | ……………………… |
| (e) Gharama za awali | ……………………… |
| (f) Mengineyo | ……………………… |
| (g) Mtaji wa kufanyia Kazi | ……………………… |
| Jumla | ……………………… |

Mawasiliano:
Jina……………………………………Cheo……………………
Simu………………………………… Nukushi…………………………
Barua pepe…………………………

FOMU Na. 5

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 27 (2) )*

TAARIFA YA MWAKA YA MWEKEZAJI

1. Taarifa ioneshe
   (a) Mpango kazi kwa mwaka husika;
   (b) Hali ya utekelezaji wa mpango kazi mpaka tarehe ya taarifa: (mf. kuanzia tarehe ya kuthibitishwa kwa mradi mpaka tarehe ya kuwasilishwa kwa taarifa); na
   (c) Fafanua kuhusu shughuli ambazo zimetekelezwa, mfano ujenzi wa majengo, usambazaji wa vifaa, ufungaji wa mitambo, vifaa n.k.

2. Taarifa ioneshe hali ya sasa kwenye maeneo yafuatayo;

| Na. | Eneo | Ufafanuzi | Hali ya Sasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa za Wanahisa | Majina ya Wanahisa, uraia, na asilimia za umiliki wa hisa | |
| 2. | Taarifa ya Mawasiliano ya Kampuni | Anwani ya Barua pepe | |
| | | Namba ya Simu ya mkononi | |
| | | Namba ya Simu ya Mezani | |
| | | Anwani ya Makazi (Kiwanja, Kitalu, Mtaa, Wilaya na Mkoa | |
| 3. | Mawasiliano kupitia kwa | Jina | |
| | | Cheo | |
| | | Mawasiliano ya Kina (Barua pepe, Simu ya Mkononi na ya Mezani) | |
| 4. | Usajili wa Taasisi ya Biashara | Aina ya Usajili wa Taasisi ya Biashara | |
| | | Na. ya Cheti cha Usajili. | |
| 5. | Taarifa za Usajili wa TIN | Na. ya Usajili wa TIN. | |
| 6. | Malengo ya Mradi | Shughuli za Msingi za Mradi | |
| 7. | Uwezo | Uwezo wa uzalishaji wa mradi kwa mwaka | |
| 8. | Ajira za moja kwa moja zilizopo sasa | Ajira za Kigeni-Wanaume | |
| | | Ajira za Kigeni-Wanawake | |
| | | Ajira za Ndani-Wanaume | |
| | | Ajira za Ndani-Wanawake | |
